# CHEMO-CASPAR


## ANAVYOWINDA SELI ZA SARATANI



*Mtunzi wa hadithi:*
*Helle Motzfeldt*

Salaam,

Sasa ninakuletea hadithi ya bwana mmoja ait-waye Chemo-Casper na adui wake mkubwa ait-waye Seli-Saratani. Lakini kwanza nitakusimulia nini maana ya neno seli kwa kuangalia michoro hii niliyokuandalia.



Hebu iangalie vizuri, halafu uifananishe na nyumba ndogo iliyozungukwa na ngozi mithili ya kuta ama nguzo za nyumba. Huu ni mwili wa binadamu ambao ndani una vyumba, na kila chumba kina njia zake za kuingilia na kutokea.

Ndani ya nyumba hii kuna shimo dogo (tumbo) ambalo linapokea na kuhifadhi chakula unachokula. Vilevile ndani ya nyumba hii kuna chumba kingine kidogo kinaitwa moyo. Kazi kubwa ya moyo ni kusukuma damu na kuisambaza sehemu zote za mwili wako. Damu hii inazunguka mwilini kupitia ndani ya vijibomba vyembamba viitwavyo vena, ama mishipa ya damu.

Ingawa huwezi kuviona vitu vilivyo ndani ya mwili wako, lakini bila shaka mara kwa mara umewahi kusikia tumbo likinguruma. Na pia kama ukiweka kiganja chako upande wa kushoto wa kifua chako, utaweza kusikia mapigo ya moyo wakati damu inaposukumwa kwenda sehemu nyingine za mwili.




Nyumba mara nyingi hujengwa kwa matofali, kama vile ambavyo ngozi yako hujengwa kwa seli ndogondogo. Kila kiungo mwilini mwako kina seli ambazo zimepewa majina tofauti kufuatana na viungo vyenyewe. Kwa mfano, katika ngozi zinaitwa seli za ngozi, katika damu zinaitwa seli za damu, na katika nywele zinaitwa seli za nywele.

Seli hizi ni ndogo sana kiasi kwamba huwezi kuziona. Ndiyo sababu nimekuchorea mifano ya baadhi ya seli hizo ili uweze kuziona zilivyo mwilini. Je, ukiangalia michoro hii unaweza kuzitambua seli za nywele? Ni vigumu kuelewa seli ni nini wakati huwezi kuiona, lakini jaribu kufikiria na kuelewa kwamba seli katika ngozi yako ziko karibu sana kama vile matofali yalivyo kwenye ukuta wa nyumba. Ndani ya mishipa yako ya damu, seli za damu zinaelea na kusambaa mwilini pamoja na seli nyingine za damu. Uliwahi kuumia katika ngozi na kutokwa na damu? Elewa kwamba katika damu hiyo kulikuwa na seli nyingi za damu.



Seli zote mwilini ni nzuri kwa sababu zinaelewana na kupendana, na zina maeneo ya kutosha ya kuishi mwilini. Unaweza kuona katika mchoro huu kwamba seli huwa zinazaa seli nyingine ndogo ambazo baadaye zinakuwa kubwa. Hivyo basi, kadiri seli za mwili zinavyoongezeka, vilevile zitahitaji eneo kubwa zaidi la kuishi mwilini. Ndiyo sababu binadamu naye anakua mkubwa siku hadi siku tangu kuzaliwa.



Hata hivyo, kuna wakati inatokea kwamba kuna seli moja mwilini ambayo itazaa seli nyingine ambayo haifanani na wenzake kitabia. Seli hiyo changa ni mbaya sana kiasi kwamba haizipendi seli nyingine mwilini; kila wakati inapenda kuishi peke yake. Seli hii inaitwa seli ya saratani. Unaiona ilivyo mbaya hata kwa sura katika mchoro huu? Hii ndiyo seli inayosababisha ugonjwa wa saratani.



Seli nyingine hazifurahishwi na mwenendo wa seli hii ya saratani kwa vile inawasukuma na kuwasumbua sana. Lakini seli hiyo ya saratani haijali kitu, bali inazidi kuzaa seli nyingine mbaya za saratani, na hatimaye kufanya idadi ya seli hizo mbaya kuwa kubwa zaidi.



Seli hizi za saratani zinajikusanya na kutengeneza uvimbe katika sehemu mbalimbali za mwili na kupunguza maeneo ya kuishi ya seli nyingine nzuri za binadamu. Seli hizi nzuri zinakasirika sana kuona seli za saratani zikizidi kuongezeka kila siku. Kama nilivyokwisha kueleza hapo awali, seli za saratani wakati mwingine zinasababisha uvimbe ndani na nje ya mwili; na ikibidi uvimbe huo lazima ukaondolewe na daktari hospitalini. Je, uliwahi kupata uvimbe kama huo na kwenda kutibiwa hospitalini?



Kwa bahati nzuri kuna baadhi ya seli nzuri za damu ambazo zina nguvu na uwezo wa kupambana na kuziua seli mbaya za saratani. Katika michoro niliyokuandalia unaweza kuona jinsi seli zako nzuri za damu zinawyoishambulia kichwani seli mbaya ya saratani. Inashambuliwa kwelikweli huku seli nzuri za damu zikifurahia kuchapwa kwa seli hiyo ya saratani.

Kama unavyoona, siyo kazi rahisi kuishambula na kuiua seli ya saratani, lakini hata hivyo seli zako nyingine za damu zinaweza kupata msaada wa kuiangamiza seli hiyo mbaya ya saratani. Msaada huu unatoka kwa mwindaji mashuhuri wa seli za saratani aitwaye Chemo- Casper ambaye kila wakati yuko tayari kutoa msaada kama huo kwa seli nzuri za damu. Sasa sikiliza kisa kifuatacho.




Chemo- Casper yeye anaishi hospitalini. Daktari huwa anamtafuta pale anapoishi ndani ya chupa na rafiki zake wengine. Siku moja daktari alimjia Chemo- Casper na kumuambia: "Leo ninakutuma kwenda kufanya kazi. Nimejiwa na mgeni, mtoto mdogo ambaye anahitaji msaada wako ukaziondoe mwilini zile seli mbaya za saratani ambazo zimekwisha kuanza kujenga uvimbe kwenye sehemu za mwili wake. Seli zake mwenyewe za damu zinajitahidi sana kupambana na seli hizo mbaya za saratani, lakini kwa kweli bado anahitaji msaada wako."

Chemo- Casper akajibu: "Sawa daktari, tuko tayari kuifanya hiyo kazi. Twendeni tukaianze bila kuchelewa."



Ndipo daktari akachukua bomba la sindano na kuwajaza ndani ya bomba hilo Chemo- Casper na rafiki zake wote, na kuharakisha kwenda kwa mtoto mgonjwa.



Walimkuta mtoto huyo aitwaye Joachim amelala kitandani akimsubiri daktari na jeshi lake la Chemo-Casper. Mtoto huyo alijifunika shuka gubigubi (mwili mzima) kwa sababu alikuwa anaogopa, hakujua nini kitakokea. Joachim hakuweza kumuona Chemo- Casper na wenzake ndani ya bomba la sindano kwa vile ni wadogo sana, kama vile seli za damu.



Chemo- Casper alikuwa wa kwanza kupenyeza mwilini mwa mgonjwa wakati daktari alipomdunga sindano Joachim. Wakati anatimua mbio kwa viguu vyake vidogo ndani ya damu ya Joachim, akawa anawaita askari wenzake: “Njooni, kimbieni, nifuateni, haraka…” Seli za Joachim zilifurahi mno kumuona Chemo- Casper na jeshi lake: “Tunashukuru sana kwa kufika kwenu. Tusaidieni kuwakamata hawa seli wabaya wa saratani. Wanatunyanyasa sana”.

Seli za saratani hazikufurahia ujio wa jeshi la Chemo- Casper. Zilijificha na kujaribu kuwakimbia askari hao wakali.



Lakini wakazuiwa na kuanza kuliwa mmoja baada ya mwingine. Wakati wote huo, seli za damu za Joachim zilikuwa zikifurahi na kushangilia, huku Chemo- Casper na wenzake wakizidi kuwacharanga seli wabaya wa saratani.



Kuna wakati askari wa Chemo- Casper hawaoni vizuri. Ndiyo sababu katika mchoro huu unawaona wamevaa miwani ili wapate kuwaona vizuri maadui zao. Saa nyingine miwani hizo huwadondoka, na hivio huzing`ata na kuziua kwa bahati mbaya seli nzuri za Joachim.




Angalia mchoro huu uone ni jinsi gani askari wa Chemo- Casper walivyokosea kwa bahati mbaya na kuzishambulia seli za nywele za Joachim. Mwaangalie Joachim anavyoshangaa kuona nywele zake sikinyonyoka wakati akizishika. Ni jambo la kushangaza kuona nywele zako zikingonyoka bila kujua sababu, kumbe kuna adui anazinyemelea. Hata hivyo, nywele hizo zinaweza kuota tena kama makovu ya kung`atwa yakipona kutokana.



Na kazi kubwa inayafanywa na Chemo- Casper na askari wenzake. Kuna wakati pia seli za saratani hushambulia tumbo la mgonjwa, kama Joachim, na halafu akapata kichefuchefu na kutapika.



Vita inachosha sana. Kuna wakati Chemo- Casper na askari wake huwa wanachoka na kuishiwa nguvu. Basi inabidi waondoke mwilini mwa Joachim na kurudi kwao kutafuta nguvu nyingine. Wakati wa vita kama hii, kuna maadui (seli za saratani) wengine hujificha vizuri sana kiasi kwamba hata Chemo- Casper na wenzake hawawezi kuwaona. Ndiyo maana Joachim inambidi arejee hospitali mara kwa mara kukutana na jeshi la Chemo- Casper hadi seli zote mbaya za saratani ziangamizwe na kupotea kabisa.



Kama umeipenda hadithi hii unaweza kufumba macho yako na kufikiria namna gani Chemo-Casper na rafiki zake, na seli zako mwenyewe ndani ya damu, zinavyosaidiana kupambana na seli mbaya za kansa.

*Mtunzi wa hadithi: Helle Motzfeldt*

*Tafsiri ya Kiswahili: Doris Kibula Rajabu na Revenant Muro, Tanzania.*

*Imechapishwa kwa msaada wa “BarnsBeste” na “Soerlandet hospital”, Norway - www.barnsbeste.no*

*Shukrani ziwaendee Helle Motzfeldt na ”Familier med kraeftramte born”, Denmark, kwa kuridhia tafsiri ya kitabu chao cha mwanzo katika lugha nyingine.*

*Shukrani maalum pia ziwaendee Marit Kleppe na Lillian Anita Warberg, Norway, wanaofanya kazi katika Taasisi ya Saratani Ocean Road (Tanzania) na Hospitali ya Chuo Kikuu cha Haukeland (Norway) kupitia Fredskorpset (Norway), pamoja na Doris Kibula Rajabu na Revenant Muro kwa juhudi zao za kutafsiri kitabu hiki katika lugha ya Kiswahili.*

*Tunamshukuru mwandishi Helle Motzfeldt na shirika la ‘Familia za watoto wenye saratani’ ya Denmark bila malipo, mshika dau ameiwezesha kuwepo kwa toleo halisi la Kidenish.*

*Hatimiliki:*
*Familier med kraeftramte born, Denmark.*
*Barua pepe: info@fmkb.dk*
*Tovuti: www.fmkb.dk*

